


# JOYCE MEYER

KUJIFUNZA KUTEGEMEA WAKATI UFAAO  
WA MUNGU



Lini,  
Mungu,  
Lini?

# LINI, MUNGU, LINI?

---

Kujifunza Kutegemea Wakati Mwafaka  
wa Mungu

JOYCE  
MEYER



JOYCE MEYER  
MINISTRIES

P.O. Box 5, Cape Town 8000

Maandiko yote yaliyoonyeshwa ila tu unapoelezwa, yametolewa katika Tafsiri ya Union ya Biblia.

Maandiko yaliyo na alama (AMP) yametolewa katika Biblia ya kiingereza inayoeleza maandiko kinaganaga (Amplified Bible).

English copy  
When, God, When?  
Learning To Trust God's Timing  
ISBN 0-89274-846-X  
Copyright © 1994 by Joyce Meyer  
Joyce Meyer Ministries  
P.O. Box 655  
Fenton, Missouri 63026

Swahili Translation  
Lini, Mungu, Lini?  
Kujifunza Kutegemea Wakati Mwafaka  
Wa Mungu  
Nairobi Lighthouse Church  
P.O. Box 34041-00100  
Nairobi, Kenya

# YALIYOMO



## *Utangulizi*

1. Wakati Ufaao Na Kuamini
2. Msimu Mwafaka
3. Wakati Ulioteuliwa
4. Mwito
5. Upako
6. Kuwekwa Wakfu
7. Je, Umechoka Kungoja?
8. Subira, Tafadhali!
9. Ndoto Yangu Itatimia Lini?

Jinsi Ya Kupokea Maisha Mapya

Kuhusu Mwandishi

# UTANGULIZI



Tunamtumikia Mungu Mjua-Yote Anayetutazama wakati wote. Mungu hashangazwi na lolote. Anajua kila kitu *kabla* hakijatendeka. Zaburi 139 yasema anayajua mawazo yetu kabla hata hatujayawaza, na maneno yetu ambayo hatujayajatamka bado. Wengi wetu tunahitaji kukua katika eneo la Kumwamini Mungu na kujaribu kunyamazisha swali hili kubwa la – LINI?

Kwa sababu swali hilo ni swali linalotukumba mara kwa mara, nimeandika kitabu hiki ili kuleta kuelewa kule ninahisi Mungu kwa neema Yake Ameshiriki nami. Niliishi sehemu kubwa ya maisha yangu nikiwa mtu asiye na subira, aliye na masumbuko mengi pamoja na kutotosheleka. Kutokana na yale niliyoyapitia, nimejifunza kutegemea Yule Ajuaye yote.

Ni ombi langu kwamba roho yakoitapokea amani jinsi unavyopumzika katika Yeye, ukiamini kwamba, kwa matamshi ya Mfalme Daudi, “nyakati zako zimo mikononi mwake mwenye uwezo wa kutosha.” (Za. 31:15 *ikisemwa kwa njia nyingine*).

# 1



## WAKATI UFAAO NA KUAMINI

“Nilikuamini, na kukutegemea, na kuwa na uhakika ndani Yako, Ee Bwana. Nilisema, Wewe ndiwe Mungu wangu.

“Nyakati zangu zimo mikononi mwako; nikomboe kutoka kwa mikono ya adui zangu na wale wanaonifuatia na kuniletea dhiki.”

*Zaburi 31: 14,15 AMP*

Katika sura hii, mwandishi wa Zaburi ansema kwamba alimtumainia Mungu kumkomboa, na alimtegemea kufanya hivyo kwa wakati uliofaa. Kuntumainia Mungu kunahitaji tuseme, *“Nyakati zangu zimo mikononi Mwako.”*

Nimejifunza kwamba tegemeo linatuhitaji kukubali kwamba kuna maswali mengine ambayo yatabaki yakiwa hayana majibu na hivyo basi kuweka nyakati zetu mikononi mwake Mungu – tukiamini kwamba japo hatuyajui majibu yote, Yeye ayajua.

Anao wakati unaofaa kikamilifu kwa kila jambo maishani mwetu. Sote huwa tunatamani na kuamini kwamba mambo mazuri yatendeke maishani mwetu, *SASA – si baadaye!*

Tunavyoendelea kukomaa katika maisha yetu ya Kikristo, tunajifunza kuaminia vitu sio *SASA*, lakini katika wakati mwafaka wa Mungu. Waiberania 11:1 inasema, “Basi imani ni kuwa na hakika

ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana. Wakati wowote tunaweza kuwa na imani 'sasa', lakini sio kila wakati tutaweza kuona udhihirisho wa yale tunayo yaaminia *sasa*.

Kumtumainia Mungu mara nyingi kunahitaji kutofahamu *jinsi* Mungu atakavyo timiza yale yanayohitaji kutimizwa na pia kutofahamu ni *lini* atakavyofanya hivyo. Sisi husema, "Mungu hachelewi," lakini mara nyingi yeye haji mapema pia. Kwa nini? Kwa maana Yeye hutumia nyakati hizo kuimuda imani yetu ndani yake, na kutufanya tukakua wakati wa kungoja.

Mojawapo wa wale wanaoshirikiana na huduma yetu kifedha kila mwezi hivi maajuzi alijipata na haja ya kifedha ili aweze kulipa kodi zilizotokea ghafla, hakuzitarajia. Kodi zenyewe ilipasa zilipwe kufikia tarehe 15 Aprili.

Mume na mke huyo walitoa sadaka maalum kwa huduma ya Life In The Word wakiamini Mungu awape muujiza waliohitaji. Tarehe 14 Aprili walipata pesa za kulipa kodi ile. Mbona muujiza haukuwafikia tarehe 1 au 5 Aprili? Ni kwa nini mara nyingine Mungu hungoja mpaka siku au dakika ya mwisho kabisa?

Sababu ni kwamba yeye anatumia masomo kuhusu kumtumainia na kumtegemea. Kutumainia hakupokelewi kama urithi, huja kwa kujifunza. Tunajifunza kumtumainia Mungu kwa kupitia mabo yanayohitaji kumtegemea. Tunapouona uaminifu Wake mara moja hadi nyingine, tunawacha kujitegemea na taratibu tunaingia kwenye pumziko la Mungu na kuweka imani yetu ndani Yake.

Tukiitazama hivi, ni rahisi kuona ni vipi wakati mwafaka unavyotimiza jukumu muhimu katika kujifunza kumtumainia Mungu. Kama Mungu angefanya kila kitu tunachomuomba mara moja, hatungeweza kukua na kukomaa. Wakati unaofaa na kutumainia ni mapacha. Wanafanya kazi bega kwa bega.

# 2



## MSIMU MWAFKA

Mambo Ya Walawi 26:4 inasema, “Nitazinyezesha mvua zenu kwa nyakati zake.” Wagalatia 6:9 kwa tafsiri ya AMP inasema ni lazima “...tusife moyo na kuwa wachovu na kuzimia katika kutenda kiungwana na kutenda yaliyo ya haki, maana kwa wakati wake na kwa msimu ulioteuliwa tutavuna, kama tusipouachilia na kupunguza ujasiri wetu na hapo kuzimia.” Na katika 1 Petro 5:6 tunatiwa moyo “kujinyenyekeza chini ya mkono wa Mungu wenye nguvu, ili wakati wake ufaao utakapotimia” atatuinua.

*Msimu mwafaka au wakati ufaao ni lini? Naamini ni wakati Mungu anajua kuwa tuko tayari, wakati ambapo kila mtu anayehusika ako tayari na wakati jambo hilo linaingia vizuri katika mpango mkuu wa Mungu unaojumlisha mabo yote. Mungu anao mpango wa kipekee kwa maisha yetu binafsi, lakini pia anao mpango wa jumla kwa ajili ya ulimwengu wote.*

Nakumbuka kulikuwa na wakati ambao nilikuwa nimejawa usumbufu kwa sababu kulikuwa hakuna chochote kinatendeka katika huduma yangu. Nilijua kwamba Mungu alikuwa amenitia mafuta nifundishe Neno lake, lakini kamwe kulikuwa hakuna milango yoyote inanifungukia. Nilijihisi kuwa tayari. Nilikuwa ninaambatana na Mungu. Alikuwa amefanya kazi kuu ndani yangu na sikuelewa ni kwa nini hakuna chochote kilichokuwa



kinatendeka. Nakumbuka nikuliza, “Mungu, unangoja nini sasa? Kwani siko tayari bado?” Alinijibu kwa kusema, “U tayari, lakini baadhi ya watakaohusika pamoja nawe hawako tayari, na ningali ninakamilisha mambo kadhaa ndani yao, kwa hiyo lazima uwangoje wao sasa.”

Wajua Mungu hasukumi, wala kuseta, kushurutisha, kutumia ujanja au kulazimisha watu. Yeye hutangulia, hongoza hunong’oneza na hushauri. Ni wajibu wa kila mtu kumpa Mungu hiari yake kwa ajili ya maksudi ya Mungu. Kufanya hivi humchukua mtu mmoja muda mrefu kuliko mtu mwingine.

Kwa hivyo, ikiwa Mungu anakuza kikundi cha watu au timu ya watu watakao fanya kazi pamoja, sehemu moja ya timu hiyo wanaweza kuwa tayari mbele ya wengine.

Jambo hili hasa huwa gumu maana katika kiwango cha uzalishaji, hawaujui mpango wa Mungu, na mara nyingi hata hawafahamiani.

Mfano murwa wa haya ni mtu kijana nayemwomba Mungu kupata mchumba aliye kamilika. Wakati Mungu angali hakika anamtayarisha mchumba huyo, yule anyeomba anachoka kungoja maana hajui ni yapi yanayoendelea nyuma ya yale yanayoonekana. Kijana anayeomba kumpata mchumba aliye mkiristo aliye kommaa, ambaye amekuwa katika tunda la Roho na aliye na mwito wa kumtumikia Mungu katika huduma, na kadhalika, itambidi awe tayari kusubiri kupata agizo hilo “maalum” likiwa limepambwa vilivyo wakati wa kulipokea. Itachukuwa muda kupokea hayo. Haifanyiki kwa usiku mmoja. Hata hivyo, Mungu bado amemwekea mtu wa kumfaa.

Dave alinipata upesi, lakini ombi lake halikuwa la kudai mambo mengi. Alimwomba Mungu ampe mke, wa kumfaa, na alimwomba Mungu mke huyo awe mtu anayehitaji usaidizi. Aliomba mara moja moja kwa muda wa miezi sita hadi mwaka mmoja. Hatimaye tulikutana, tukawa na nyakati za kukutana pamoja kuchumbiana

mara tano na tukafunga ndoa.

Tumeishi kama mume na mke kwa muda wa miaka ishirini na nane kufikia wakati wa kuandikwa kwa kitabu hiki mwaka wa 1994. Dave wakati wote amesema alijua mimi ndiye niliyemfaa tangu siku ya kwanza tulipokutana kufahamiana, lakini alingoja kuniuliza kuolewa naye kwa sababu hakutaka kuniogofya.

Alifikia uamuzi baada ya wiki tatu tu za ndoa yetu kwamba nilikuwa na shida kadhaa na nilihitaji msaada mwingi. Dave alipokea jibu la maombi yake haraka, lakini ilimbidi kuvumilia nyakati nyingi ngumu nilipokuwa nikikua katika Bwana na kuyashinda matatizo yaliyotokana na maisha yangu ya kale aliyokuwa ya kutendwa isivyofaa.

Mungu alikuwa anajua kwamba Dave alikuwa amekomaa vyakutosha kuweza kustahimili miaka hiyo ya ugumu pamoja nami; kwa hivyo alijibu maombi ya Dave haraka. Alikuwa na nguvu za kutosha kuweza kumsaidia mtu aliyekuwa na shida nyingi. Dave alikuwa tayari kutumiwa na Mungu kwa njia hiyo, na Mungu alimtumia.

Kama hangekuwa tayari au kama angeomba kumpata mtu mwenye amekamilika zaidi, naamini Mungu angechelewesha jibu lake kwake mpaka wakati bora zaidi, baada ya Bwana kufanya mambo kadha wa kadha makuu katika maisha yangu kunifikisha mahali ambapo Dave alikuwa ameomba.

Ninalojaribu kusema ni kwamba wakati tunapomngojea Mungu, ni muhimu kutambua ya kwamba Mungu anaweza kuwa anakamilisha mambo kadhaa katika maisha ya watu kadhaa ili kujibu ombi letu. Kuamini hivyo kunafanya kuvumilia kungoja kuwa afadhali kidogo.

Hebu tufikirie juu ya *wakati ufaao* katika mabo ya kifedha. Waraka wa Yohana wa tatu mstari wa 2 unasema, “Mpendwa,

ninakuombea ufanikiwe katika mambo yote na kwamba uwe na afya njema ya mwili, *kama vile roho yako ifanikiwavyo.*” Sehemu ya andiko hili isemayo *kama vile roho yako ifanikiwavyo* inatufanya kuelewa kwamba ufanisi utokao kwa Mungu kunategemea kukomaa kwetu. *Kama vile roho yako ifanikiwavyo* inahusu ni kasi gani tutamruhusu Mungu kuleta nia yetu, hiari na hisia zetu kuwa sambamba na mapenzi Yake.

Harakati ya kukomaa huchukuwa muda. Kiasi cha muda huo kinategemea mpango wa Mungu na jinsi tutakavyo shirikiana na mpango huo. Mungu anatupenda sana kiasi cha kwamba hawezi kutufanikisha na fanaka ambazo hatujakomaa vya kutosha kushughulikia. Ndiposa antuambia katika Wagalatia 6:9, “Basi tusichoke kutenda mema, kwa sababu kama hatutachoka, tutavuna kwa wakati ufaao.” *Wakati ufaao* ni wakati Mungu anajua tuko tayari, sio wakati *tunafikiri* tuko tayari.

Baraka nyingi mapema mno zinaweza kumfanya kuwa na kiburi, ndio maana Biblia inatufundisha tusimweka mtu mchanga kiroho katika uongozi. Hajakomaa vya kutosha, na hayo yatamfanya kujiinua na kiburi. (1 Timotheo 3:6)

Kuna wakati mwafaka kwa kila jambo maishani mwetu, na kuna *usalama* kuwa katika wakati kamili wa Mungu. Mimi huomba kuwa katika mapenzi ya Mungu kamili kwa ajili ya maisha yangu na pia kuwa katika wakati wake wa kamili – si hatua moja mbele Yake wala hatua moja nyuma.

# 3



## WAKATI ULIOTEULIWA

Yesu aliwaambia wafuasi wake katika Matendo ya Mitume 1:6-8, walipokuwa wanamuuliza maswali kuhusu nyakati za mwisho ya kwamba haikuwa juu yao kujua siku za usoni zitaleta nini wala misimu ambayo Baba alikuwa ameiteua kulingana na kuchagua kwake na kwa nguvu zake binafsi.

Wafuasi wake bado walikuwa wanafikiri kwamba Yesu angeanzisha na kuimarisha ufalme wa kiulimwengu. Waliuliza ni lini atakapouthibitisha ufalme tena na kuurudisha kwa Israeli.

Yesu alikuwa bado hajafaulu kuwafikisha kiwango cha kuelewa kwamba ufalme wake ulikuwa ni ufalme wa kiroho, na kwamba ufalme wake utakuwa dani yao. Biblia inatuonya kwamba maarifa bila hekima ni hatari. Ingekuwa mkasa mkuu Yesu kuwaambia wafuasi wake ni lini angelithibitisha ufalme wake na huku hawajaelewa ufalme huo ni nini.

Mara nyingi tunahitaji maelezo kuhusu *lini*, na Mungu hatuelezi kwa sababu hatuna hekima ya kutosha kuambatana na maelezo hayo. Habakuki 2:3 (Tafsiri ya AMP) inasema, “Maana njozi hii bado ni kwa wakati ulioamriwa, inafanya haraka ili kuufikilia mwisho wake [kutimilika]; wala haitasema uongo au kutotimia; ijapokawia, ingojee [kwa makini] kwa kuwa haina budi kuja, haitakawia; haitakuwa nyuma ya wakati iliyopangiwa.”

Haitachelewa hata siku moja.

Maana ya *Wakati ulioamriwa* ni wakati ule Mungu anajua tuko tayari. Lazima tunyenyekee mbele zake na kunyenyekeza mawazo yetu pia kwa hekima na nguvu zake na kumwamini anaposema kwamba hatachelewa.

*Wakati ulioamriwa* pia inamaanisha wakati ulioteuliwa na uamuzi kufanywa kuuhusu kwa ajili ya sababu fulani. Ni kama kupewa mwaliko wa saa fulani mahali fulani. Hatuwezi tukaingia mahali hapo mpaka saa zile zimetimia, na hivyo ndivyo ilivyo. Mungu anao wakati aliouteua, ama tunaweza kusema ametupa mialiko kuhusu mambo fulani maishani mwetu, na mialiko hiyo ni ya wakati fulani. Afadhali tu tutuliena tungoje kwa subira kwa sababu huo ndio wakati mambo hayo yatatendeka na wala sio mbeleni.

# 4



## MWITO

Wakati wa Mungu kumwita mtu afanye jambo fulani, kisha kumpa upako wa kufanya hivyo na zaidi ya hapo kumweka wakfu kufanya kazi hiyo unaweza kuwa, na mara nyingi huwa katika sehemu tatu tofauti. Mara nyingi kuna nyakati refu kati ya matukio hayo, hasa kama mtu huyu anaenda kutumiwa na Mungu kwa njia kuu. Kutumiwa na Mungu kwa njia kuu siyo kwamba inamaanisha ulimwenguni kote. Inamaanisha tu kwamba ni kwa njia itakayo husisha kiasi kizuri cha watu. Katika sura hii, na zile mbili zifuatazo, tutatazama matukio haya matatu kila moja kivyake.

Mungu anapoweka mwito katika maisha ya mtu fulani, ni jambo linaloweza kutendeka ghafla, au inawezekana ni jambo ambalo mtu huyo anaweza kuwa amejua kwa muda mrefu. Nakumbuka nikisoma kwamba mojawapo wa marais wa nchi ya Marekani alikuwa amesema alipokuwa akihojiwa kuwa tangu utotoni mwake alikuwa, anaishi na tamaa na “kujua tu” kwamba siku moja atakuwa rais wa nchi ya Amerika.

Mwito wangu ulinijia kwa njia ya ghafla. Nikuwa nikitandaza kitanda changu asubuhi moja, na sauti ya Bwana ikanijia ikisema, “Wewe utanenenda kila mahali ukifundisha neno langu, na utakuwa na huduma kubwa ya kanda za mafundisho.” Ingawa haikuwa sauti inayoweza kusikika na masikio, ilisikika kama sauti ya juu

na wazi kabisa ndani yangu. Na kutoka wakati huo na kuendelea, “nilijua tu” kwamba huo ndio mwelekeo wa maisha yangu, na nilikuwa ninatamani kwa hamu kuu kulifundisha neon la Mungu. Wakati mwingine hamu hii ilikuwa karibu kunilemea.

Kabla ya siku hiyo sikujua kwamba nilikuwa na mwito wa kuhubiri na kulifundisha Neno la Mungu. Lakini ninapoangalia nyuma sasa, ninaweza kuona ilani kadhaa katika njia ya maisha yangu. Nilikuwa nina uwezo wa kujieleza vizuri na kwa njia ya kueleweka katika maongezi yangu na katika yale niliyoyaandika. Hata nilipokuwa katika shule ya upili, watu walinijia wakihitaji msaa, pia na ushauri katika shida zao. Nilikuwa na tamaa hata wakati huo kusaidia watu kunyorosha maisha yao. Niliombwa hata kutoa hotuba ya kwanza katika siku ya kufuzu kwangu kutoka shule ya upili, ili kuwatia motisha wanafunzi wenzagu na kuwapa msukumo wa kuyatazamia makuu siku za usoni.

Hata nilifikiri kurudi chuoni ili kupata digrii katika saikologia ili kuweza kuwasaidia watu kama mtu aliyehitimu.

Baada ya Dave na mimi kuishi pamoja katika ndoa kwa miaka mingi, niliendelea kukua na kumkaribia Bwana lakini bado nilikuwa ninapambana na shida kuu kutokana na maisha yangu ya kale ya kutendwa isivyofaa. Kufikia sasa tulikuwa na watoto watatu, na ninakumbuka nilikuwa ninatoka kanisani kila juma pili jioni na kulala kitandani baada ya watoto kulala. Wakati huo nyumba ingelikuwa iko kimya na yenye amani na giza, na nilihubiri tena jumbe za mchungaji, tofauti pekee ikiwa ni kwamba ni mimi niliyejiona nikiwa madhabahuni na wala si mchungaji. Si kujua ni kwa nini nilikuwa nikifanya hivyo, lakini sasa najua.

Mwito wako unaweza ukaja kwako kwa kipindi cha muda fulani au unaweza ukaja kwako ghafla, lakini tangu wakati unapoitwa, *uko matayarishoni.*

# 5



## UPAKO

Wakati wa matayarisho, upako huwa unawachiliwa kuingia maishani mwetu kwenye vidonge vilivyopangwa kutufikia katika wakati kamili ulioteuliwa na Mungu. Upako ni Roho Mtakatifu akituwezesha kufanya kile ambacho Mungu ametuita kufanya. Roho Mtakatifu hutufundisha, hutusahihisha, hututakasa, hutusaidia na kututia nguvu. Yeye hutuunda na kututengeneza kuwa vyombo vinavyofaa kwa matumizi ya Bwana. Hii inaweza kuchukua miaka na miaka kutekeleza.

Hebu mfikirie Musa. Alikuwa anahisi mwito wa kuwakomboa wana wa Israeli kutoka kwa maisha ya utumwa. Alichomoka na harara na kumuua mmisri aliyekuwa anamtesa mwisiraeli, na matokeo yake ni kwamba ilimbidi kuishi miaka arobaini iliyofuata sehemu ya nyuma ya jangwa akijifundisha juu ya uchungaji, akimfahamu Mungu na akinyenyekezwa. *Alikuwa anapokea ujuzi.* Mtu asiye na mafundisho, wala ujuzi na unyenyekevu hawezi kutofautisha kati ya harara ya kibinadamu na wakati uliowekwa na Mungu.

Upako huachiliwa maishani mwetu kulingana na jinsi tunavyoshirikiana na Mungu katika wakati wa matayarisho. Mfikirie Yusufu, aliyelitwa na Mungu kuwa mtawala nchini Misri ili kuokoa halaiki ya watu kutoka kwa janga la njaa. Alikuwa akiota juu ya mambo haya akiwa angali kijana. Katika ilie harara,



aliwaambia ndugu zake ndoto zake. Hawakupendezwa na wazo la kumwinamia kaka yao mdogo, kwa hivyo wakamuza.

Yusufu hakumtarajia yeyote mabaya. Alikuwa kijana mzuri lakini ni wazi kwamba hakutumia hekima alipowaambia yale aliyokuwa ameyaona katika ndoto zake. Mungu aliruhusu miaka migumu maishani mwake, lakini miaka hiyo ilimfundisha hekima. Yale aliyoyapitia yalimtararisha kutimiza mwito wake. Alipitia kusalitiwa. Si na jamii yake tu, bali pia na marafiki aliokuwa amewatendea mema akifikiria angeweza kuwaamini. Uwongo ulisemwa juu yake na alihukumiwa kimakosa na kuadhibiwa wakati hakuwa na hatia, na ilimbidi kungoja miaka mingi kabla ya kuona kutimilika kwa ndoto zake.

Sisi sote hupitia mambo kama haya kwa njia tofauti ili yatusaidie kukua. Mambo haya hututayarisha kumtumikia Mungu na kusimama imara hata iweje. Si Mungu anayetuletea shida; ni shetani. Shetani anakusudia kuleta uharibifu katika maisha yetu, lakini Mungu huipindua shida ile na kuitumia kwa njia ya kutufaidisha. Yusufu aliyafahamu haya pia maana katika Mwanzo 50:20, aliwaambia kaka zake waliokuwa wametubu kwamba, “Yale mliyoyakusudia kuniletea mabaya, Mungu alitarajia kuyatumia kwa ajili ya mema.” (*Kwa Maneno mengine*)

Mungu aliponiita kufundisha neno lake, jamii na marafiki walinikataa, nami nilikuwa mpweke na niliumizwa sana na jambo hilo. Watu walinihukumu kimakosa wakakosa kunielewa. walizungumza kunihusu kwa njia isiyo ya upole. Lakini mimi pia nilikuwa na umbele, mtu msukumizi aliyejaa harara isiyo na hekima. Kwa kifupi *nilikuwa nimejaa ubinafsi*. Naweza kuongeza kwamba kila mtu huwa amejaa ubinafsi kabla ya kupitia wakati wa matayarisho yeye mwenyewe.

Labda sasa hivi una wazo kama hili: “Si mimi – Sina shida kama hizi,” basi hebu nikushauri kwamba u njiani kupokea uamsho wa kugutusha kukuhusu wewe mwenyewe.

Na kabla hujajinyenyekeza “chini ya Mkono Wake wa nguvu”, basi wakati wako ufaao hutawahi kuja. (1 Petro 5:6)

Nikiangalia nyuma sasa, ni wazi kwamba nyakati tulipiga hatua za kwenda mbele katika huduma ya Life in the Word ziliambatana na nyakati za kukua kwangu katika Bwana na kuongezeka kwa upako maishani mwangu.

## **Vikundi vya Kujifundisha Biblia Nyumbani**

Katika mojawapo ya hatua za kwanza Mungu alinielekeza kuacha kazi yangu ya ajira iliyokuwa ya mshahara mzuri ili nijitayarisha kuingia katika huduma, jambo ambalo lilinichukua muda lakini mwishowe nilifanya. Uamuzi huu ulimaanisha kwamba mapato yetu yalikuwa nusu ya yale ya awali. Mungu kila wakati alikutana na mahitaji yetu, lakini hiyo ilikuwa miaka ya kipato kidogo.

Nilianza kwa kufundisha vikundi vya kujifundisha biblia manyumbani, kwa kipindi cha karibu miaka mitano. Kwa miaka miwili na nusu ya kwanza, nilifundisha mara moja kwa wiki.

Mkutano wa kikundi hicho ulikua ukawa mkubwa sana kiasi ya kwamba nilianza kufundisha mikutano miwili – wa kwanza asubuhi na wa pili jioni. Ingawa Dave na mimi tulikuwa tunapitia nyakati ngumu kifedha wakati huo, sikupokea fedha zozote kutoka kwa mikutano hiyo.

Watu tuliokuwa tukiwafundisha, kama watu ishirini na watano kwa kila mkutano, walipinga wazo lolote la matoleo yoyote kupokelewa kwa ajili yetu licha ya kwamba tulikuwa na mahitaji kadhaa ya kuonekana wazi. Niliendelea kufundisha, na ni wazi basi kwamba sikuwa nikifanya hivyo kwa sababu za kupata pesa. Ingawa ilikuwa vigumu wakati mwingine kutochukizwa na watu hao, niligundua baadaye kwamba mambo yalikuwa hivi kwa sababu Mungu hakutaka nijue riziki yangu itatoka wapi. Alikuwa

anataka kujithibitisha Yeye kuwa Mfanisi wangu, na kufanya hivyo ni jambo linalochukua muda pamoja na kustahimili mapito magumu ambayo kwetu sisi afadhali kuyakimbia.

Wengi hukimbia. Wameitwa, lakini kwa sababu hawako tayari kustahimili wakati wa matayarisho, hawapati kuchaguliwa kutoka kati ya wale walioitwa. Mathayo 20:16 (AMP) husema, “Wengi wameitwa, lakini wachache kuchaguliwa.”

Nilisikia mnenaji mmoja akisema kwamba maana ya andiko hili ni kwamba, “wengi huitwa, lakini ni wachache wanaokubali kuchukua wajibu ujao na mwito huo.”

*Tafsiri ya Amplified* hutoa maelezo zaidi katika tafsiri yake ya 2 Timetheo 2:15 kuhusu wajibu tulio nao kwa ajili ya mwito wa maisha yetu, “Soma na kujitahidi na kuwa mwadilifu kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu mtenda kazi (aliyehitimu kwa kupitia majaribu), asiye na sababu ya kutahayari, anayepambanua kwa njia sawa na kutumia kwa halali [kulitumia vyema na kulifundisha kwa ushupavu] neno la kweli.”

Katika miaka hiyo ya kufundisha watu ishirini na watano sebuleni, Mungu alinifundisha mambo mengi kuhusu huduma.

## **Kuwekwa Kabatini**

Baada ya hapo, nilikuwa na mwaka mmoja mzima ambapo sikufanya chochote katika huduma. Mungu alikuwa amenena nami akisema, “Acha mafundisho ya Biblia manyumbani; tazama, nafanya jambo jipya.”

Tamaa yangu ya kufanya mafundisho hayo ya Biblia manyumbani ilikuwa imeshatoweka! Nilikuwa na mtoto mchanga, na kila kitu katika moyo wangu, na hata katika mazingara yangu, yalitia nguvu na kuhakikisha neno hilo kutoka kwa Mungu.

Kwa njia moja, ilikuwa ni vigumu kutii. Wale watu hatimaye walikuwa wameanza kutupatia sadaka ndogo kila wiki. Kwa kawaida ilikuwa kati ya dola kumi na tano na dola hamsini. Hata hivyo kupitia mwezi mzima, matoleo hayo yalikuwa yanatusaidia sana. Sasa ilibidi niwe tayari kukubali kuiacha njia hiyo ya kupata riziki ili niweze kuchukua hatua iliyofuata.

Katika mawazo yangu ya kimwili nilitarajia mambo kabambe kutendeka baada ya kutii kwangu kulikoambatana na kujinyima hivyo; ukweli ni kwamba, *hakuna chochote kilichotendeka kwa muda wa mwaka mmoja!* Hakuna milango iliyofunguka!. Kwa njia nyingi, huu ndio uliokuwa mwaka mgumu kabisa katika maisha yangu. Je, nilikuwa nimekosa mwongozo wake Mungu? Je, yale niliyoyatarajia yangetendeka kweli? Ningefanya nini kuyafanya yatendeke? Mungu alishinda akisema, “Acheni, mjue ya kuwa mimi ni Mungu” Zaburi 46:10).

Mara nyingi ni vigumu sana kutulia na kungojea wakati ufaao uliowekwa na Mungu. Wakati huo sikuelewa ninayokueleza sasa. Sisi huweza kuelewa mambo vyema zaidi tunapoyaangalia tukiwa tumeshayapitia lakini tunayaelewa kwa kiasi kidogo sana tunapoyachuchumilia yakiwa yangali mbele yetu. Wakati mwingine Mungu huwaweka watu kabatini na kuwaacha wakae hapo tu. Inaonekana kana kwamba hakuna kitu kinatedeka, na kumbe mengi yanakamilishwa katika Roho. Ni wakati wa kukua, wa kulenga shabaha sawa sawa, wa kusafishwa na wakati wa kuendelea kuamini japo hakuna lolote linaloonekana.

## **Miaka Mitano Iliyofuata**

Kuelekea mwisho wa mwaka huu wa kungoja, Dave pamoja nami tulianza kushiriki katika kanisa jipya liliokuwa limeanza tu katika eneo la St. Louis. Lilikuwa kanisa dogo lilokuwa na watu kama thelathini hivi, lakini tulikuwa na uhakikisho mkuu katika mioyo yetu kwamba Mungu alitaka tuwe pale. Baada ya kuwa pale kwa

muda, nilipewa fursa ya kuanza 'Mkutano wa Kina Mama' kila Alhamisi asubuhi hapo kanisani Life Christian Center.

Mkutano huo ndio uliokuwa umwekwa wakfu na Mungu kwa kipindi cha kufuata katika huduma yangu, na yote haya yalikuwa yanafanyika *kwa wakati wake Mungu*.

Jinsi Mungu alivyoendelea kubariki, ndivyo mkutano huu uliendelea kukua. Katika kilele chake, tulifurahia kuwa na kina mama mia nne wakihudhuria kila wiki. Mwishowe niliajiriwa na kanisa hiyo na kuhudumu kama mchungaji msaidizi. Niliwekwa wakfu kufanya kazi ya huduma kupitia kwa huduma ya Life Christian Center na nikafundisha chuo cha Biblia hapo. Baadaye kanisa ilidhamini kipindi changu cha kwanza cha redio iliyokuwa ikitangaza hapo St. Louis.

Nilijifunza mambo mengi makuu wakati wa miaka yangu mitano hapo. Mojawapo ya mambo niliyojifunza ni jinsi ya kunyenyekea kwa yule aliye na mamlaka juu yako. Mtu hafai kuwa kwenye mamlaka kama hajapitia kuwa chini ya mamlaka. Kumbuka, kunyenyekea si tendo tu, ni nia inayoambatana na tendo hilo pia. Unaweza kuamua kufanya kile unachoambiwa kufanya, lakini hiyo haitoshi. Nia ya kunyenyekea lazima izaliwe ndani yako, hasa kama wewe ni mtu asiye badili maoni yako kwa urahisi, kama nilivyokuwa mimi.

Baada ya muda nilijifunza jinsi ya kufanya kazi pamoja na kikundi cha watu na pia kutekeleza wajibu wangu katika huduma za aina mbali mbali. Pia nilijifunza mengi zaidi kuhusu kungojea. Kulikuwa na mambo mengi ambayo Mungu alikuwa ameyaweka moyoni mwangu, mambo ambayo nilataka kuyafanya, lakini, kwa mara nyingine tena, wakati haukuwa wa kufaa – na basi ikawa ni kungoja zaidi, kujifunza zaidi na kukua zaidi.

Hii ilikuwa ni miaka mizuri, na ilikuwa miaka migumu iliyojaa furaha na machozi, kulisimka na kushushwa moyo. Kupitia

mambo hayo yote, wachungaji wa Life Christian Center, Rick na Dona Shelton, pamoja na Dave na mimi tulifanyika, na bado tungali, marafiki wa chanda na pete. Sote tulikua pamoja.

Nimejifunza kwamba watu wanapokua pamoja, kama hawata kata tamaa ya kuendelea pamoja, huwa wanaungamanishwa pamoja katika uhusiano wa kina kirefu utakaodumu hata wakati wote. Unaweza kuieleza hivi, uchafu ukiwa unapondwa kutoka kwenu, ndivyo mnavyoendelea kuungamanishwa pamoja.

Wakati Life Christian Center ilikuwa imekua kufikia watu 1,200, watenda kazi wa pale kanisani walikuwa wako tayari kuingia kwenye jengo jipya la kanisa lililokuwa maridadi kabisa. Mambo yote yalikuwa yanalipuka na ushindi na msisimko wakati Mungu aliponena tena.

# 6



## KUWEKWA WAKFU

### **Huduma ya “Life In The Word” Yaanza**

Unakumbuka wakati Mungu aliponena nami awali? “Mwito” ulikuja kwangu nikiwa nakitandaza kitanda changu, na Bwana akasema, “Utaenenda kila mahali... na kuwa na huduma kubwa ya kanda za mafundisho.” Hayo yalikuwa yametimizwa kwa kiasi kidogo katika miaka ya matayarisho, lakini maono yalikuwa yameongezeka katika sehemu zingine.

Siku moja nikiwa kwenye maombi, andiko fulani lifunuliwa kwangu katika Wafilipi 2:16 kwa njia kuu. Lilisema hivi (Tafsiri ya AMP), “Mkiushikilia (ulimwengu), na kuwatolea [watu wote] Neno la Uzima...” Siku hiyo nilipokea maono ya kuifikia nchi yote nzima kupitia kwa redio.

Sikuwa nasikika kwenye kituo chochote cha redio wakati maono hayo yalipokuja. Nilikuwa nimesafiri kidogo lakini si mabli sana.

Kulikuwa na matarajio zaidi katika moyo wangu, lakini nilikuwa nikifiri kwamba, kwa njia yoyote ile, Mungu angeyaingiza yote haya na kuyatimiza kupitia kwa kazi yangu pale Life Christian Centre, ambayo nilikuwa naipenda sana. Lakini Mungu alikuwa na mipango mingine.

Mithali 16:9 inasema, “Moyo wa mtu huifikiri njia yake, Bali Bwana huziongoza hatua zake.” Nilikuwa na mpango. Nilifikiri ulikuwa ni mpango wa Mungu, lakini alinizungumzia tena na kusema, “Nimetimiza lengo langu la kukuleta hapa. Chukua huduma yako ukaende Kaskazini, Kusini, Mashariki na Magharibi.” Niliona katika Roho kwamba nilikuwa niuchukue mkutano uliokuwepo wa Life in the Word uliotekelezwa katika maskani ya Life Christian Center na kuanza mikutano kama hiyo katika sehemu zingine.

Nilipingana na jambo hili kwa muda mrefu, lakini mwishowe nilihisi kuwa hakika ni Mungu aliyekuwa anasema nifanye hivyo. Nilijua pia kwamba ikiwa nilikuwa nimekosea, basi nigepoteza kila kitu ambacho nilikuwa nimefikia katika kipindi cha miaka kumi iliyopita. Nikawa na hofu!

Hatimaye nilimtii Mungu na kuacha kazi yangu pale kanisani. Ni wakati huu wa mpito ambapo Mungu alinionyesha kwamba alikuwa ananiweka wakfu kwa “mwito” uliokuwa juu yangu. Yale yote yaliyokwisha tendeka yalikuwa mazuri ajabu, lakini yote hayo yalikuwa ni matayarisho. Kwa kila hatua katika safari hii, upako wake Mungu uliongezeka kadri wajibu wangu ulivyoongezeka.

Katika Matendo ya Mitume 13:2, imenakiliwa kwamba wateule walipokuwa “wanamfanyia Bwana ibada” pamoja, Roho Mtakatifu aliwaambia wamtengee “sasa” Paulo na Barnaba kwa ajili ya kazi aliyokuwa amewaitia. Walikuwa wakifanya mambo mengi katika huduma, mambo ya kuleta mazao mema na yaliyokuwa yameleta baraka. Lakini katika wakati ufaao wa Mungu, Yeye Alisema, “SASA ndio wakati ulioamriwa.”

Nataka nikutie moyo kwamba katika wakati ufaao ulioteuliwa na Mungu, utaona ndoto na maono uliyopewa na Mungu yakitimia. Kama Ameweka mwito fulani katika maisha yako, Atautimiza katika wakati aliouteua. Shirikiana Naye kila hatua ya safari hii na kumbuka kwamba mwito, kupokea upako na kuwekwa wakfu



kwa ajili ya mwito huo, yote haya yawezeka kutendeka kupitia kipindi cha miaka mingi.

*Kuwa mwaminifu katika mambo yote madogo madogo. Nyakati zako zi mikononi mwake.*

# 7



## JE, UMECHOKA KUNGOJA?

Kama umekuwa ukingoja kwa muda mrefu na hujaona ukipiga hatua za kwenda mbele, haikosi unaanza kuwa mchovu sana wa kungoja. Nataka kukutia moyo kufanya upya nia yako kuhusu kungoja. Katika Marko Biblia 4:20-27 inasema kwamba yafaa tuwe na subira kama mkulima awekaye mbegu yake kwenye ardhi kisha anaingoja mvua ya awali na ya baadaye. Neno linaendelea kusema kwamba aingojeapo mbegu kumea, yeye huamka na kulala, na mwishowe mbegu ile humea. Naye, mkulima hajui inavyotendeka.

Mungu amenifundisha kupitia kwa andiko hili kuendelea kuishi maisha niliyo nayo sasa nikiwa ninayangojea mambo niliyo nayo moyoni kuja kuoenekana na kutimia. Tunaweza kuwa tumetilia mkazo sana kujaribu kuzalisha kilicho mbele yetu kiasi cha kwamba tunasahau kuchunga na kufurahia tulicho nacho mkononi.

Mimi nilikuwa na maono kutoka kwa Mungu miaka kumi kabla sijaanza kuyaona yakitimizwa. Katika muda wa miaka hiyo, naamini nilikosa furaha nyingi huku nikijaribu kuzalisha kitu hicho nje ya wakati ulioteuliwa na Mungu.

Tuseme mwanamke aliye na watoto watano atunge mimba na kuwa mja mzito. Kama angelijaribu kumzaa yule mtoto wa sita

katika mwezi wa kwanza wa mimba ile, hilo lingeonekana jambo la kipumbavu. Na je, kama angejishughulisha sana kumzaa yule mtoto kiasi cha kukosa kuwachunga ipasavyo wale wengine watano alio nao tayari? Tunaweza kuona kwa urahisi na wazi upumbavu wa kitendo kama hicho. Ukweli ni kwamba, watu mara nyingi hufanya jambo sawa na hilo katika hali zingine.

*Furahia mahali uliko ukingojea kufika mahali unataka kwenda!* Biblia inaposema kwamba mkulima huamka na hulala, naamini inamaanisha yeye huendelea kuishi maisha yake ya kwaida kila siku, huku akingoja shamba lake lijae mimea iliyochipuka jinsi anavyotarajia.

Siku moja, mchungaji fulani alitupokea katika uwanja wa ndege uliojaa umati wa watu. Kazi aina mbali mbali zilikuwa zinaendelea kila mahali. Vifaa vya kupanda ngazi vilikuwa na milolongo, na mikahawa ilikuwa na milolongo. Ilionekana kana kwamba popote tulipogeuka tulikuwa tunangoja tu.

Nikaona kwamba mchungaji yule alikuwa ameanza kuudhika na hali hiyo. Mara tu alinigeukia na kusema, “Nadhani unaweza kuona kwamba singojei vyema.”

Wakati wowote hatujangojea vyema, matokeo ni wazi, sio tu katika mienendo yetu inayojidhihirisha katika hisia zetu, bali pia katika miili yetu. Kungojea ni sehemu kubwa sana ya maisha, na kama kungojea kila mara huleta masumbuko moyoni, matokeo yake ni kwamba huleta wasiwasi ambayo mwishowe huidhuru miili yetu na yenye uwezo wa kuleta magonjwa. Mchungaji huyo ambaye hakuwa “anangoja vyema” alikuwa mgonjwa sana wakati huo na ugonjwa amabao dakatri alisema ulikuwa umeletwa na miaka mingi ya kuishi na wasiwasi nyingi. *Fanya upya nia yako kuhusu kungoja, nawe hutauona ugumu kungoja.*

Kusema kweli sisi hutumia muda mwingi maishani mwetu tukingojea kuliko muda tunaotumia kupokea. Baada ya kupokea

tulichokuwa tuingojea, tutaanza kungojea kitu kingine. Kama unaweza kuona ninachomaanisha, utaona kwa haraka kuwa *kungojea ni sehemu kubwa ya maisha*.

Tuseme kwa mfano upate nyongeza ya mshahara, kisha uanze kungoja nyingine. Unangoja kupata mtoto, kisha unaanza kungoja mtoto huyo awache kutumia napi na aanze kutumia surwali ndefu, na muda si muda unaanza kungoja aanze kujinunulia surwali ndefu zake yeye mwenyewe! Unangoja kununua nyumba, kisha unaanza kungoja kununua vyombo vya nyumba ile ambayo huingojei tena. Kisha unangoja kumpata msichana wa kazi ya nyumbani kukusaidia kusafisha nyumba na vyombo vyako ulivyongoja kupata. Je unaelewa ninachomaanisha?

Jifunze kufurahia kungoja, ukifahamu ya kwamba kungoja ndiko kutakakokufikisha ndoto yako. Yafaa niseme kuwa “kungoja vyema” ndiko kutakaokufikishia kwenye ndoto yako. Kutimizwa kwa ndoto hiyo, bila shaka kunatoka kwa Mungu, lakini kungoja ni kama kijana yule anayetumwa kufikisha ujumbe mahala fulani. Wakati mwingine, mtu huanza kungojea jambo fulani kutimika, lakini wakati kijana yule anayetumwa kumfikishia ujumbe anapofika, tiyari wameshaondoka na kwenda kuanza jambo lingine, na huenda wasiwepo kuona kutimilika kwa jambo hilo jipya pia.

Watu wasio na subira mara nyingi huwa hawatulii kiasi cha kutosha kuona mwisho wa mambo makuu kweli, maana mambo makuu huchukua muda mrefu kutimia kikamilifu. Mume wangu Dave kila mara husema, “*Cha haraka ni dhaifu, cha pole pole ni kizima kama kigongo.*” Kama kitu kimefanywa kwa haraka kuwafaa wale wasio na subira na wasio na uwezo wa “kungoja vyema”, huenda hakitadumu. Lakini ikiwa watu wako tayari kungojea wakati ulioteuliwa na Mungu, kitu hicho kitaundwa sawa sawa na kitadumu na kudumu kwa muda mrefu.

Mara kwa mara sisi huona “nyota zinazofyatuka” katika huduma

– watu ambao hutokea ghafla, kutoka mahali ambapo hapajulikani na muda si muda wanajulikana ulimwengu mzima, mara nyingi kwa sababu waliweza kuingia katika kikundi cha watu ambao waliwafungulia milango. Huduma kama hizi nadra husitawi. Mara nyingi hizo huwa na matatizo ya kifedha au ya kitabia kwa sababu utu wema hujengwa katika nyakati zile ngumu za kungojea, lakini wao hawakupitia wakati huo wa kujenga tabia na utu wema.

Kama mtu akiepuka nyakati zile ngumu na kufyatuka mara moja, kwa kawaida hatadumu. Marko 4:5, 6 husema kwamba mbegu ile inayoota kwa haraka kana kwamba ni kwa usiku mmoja huungua jua linapozuka. Mwishowe tunapofikia kiwango cha kukubali na kuheshimu nyakati za kungoja, Mungu huanza kufanya kazi murua kwa makini kabisa ndani yetu. Na hata ingawa hatuoni ni nini kinachotendeka, mambo yatakayo tufurahisha baadaye yanaendelea sasa hivi bila ya kuonekana.

# 8



## SUBIRA, TAFADHALI!

Biblia inasema katika Waebrania 6:12 kwamba tunarithi ahadi zake kwa imani na uvumilivu. Kupokea urithi hakuhitaji bidii yoyote kutoka kwetu. Tunahitaji kungoja tu, mpaka wakati ulioteuliwa. Kwa mfano unaweza kuamini, au kuwa na imani kwamba jamaa yako fulani amekuwosia urithi fulani, lakini ni lazima uwe na uvumilivu na kusubiri wakati ufaao kufika ili upokee urithi ule. Imani na subira ni hushirikiana katika kutimiza jambo lolote. Zinafanya kazi pamoja kutimiza lengo linalotarajiwa.

Yakobo 1:2, 3 (Tafsiri ya AMP) inasema kuwa yafaa tufurahi “tunapoangukia majaribu ya kila aina”, tukijua kwamba “kuthibitishwa kwa imani yetu” huleta saburi. Na saburi ikishafanya kazi yake kikamilifu, tutakuwa watu ambao “wamekomaa kikamilifu ... wasiopungukiwa na neno.” Jamani! Andiko la ajabu hili!

Neno la kiyunani “saburi” katika mstari huu ni neno, *hupomone*, nalo humaanisha aina ya “subira ikuayo kupitia kwa majaribu peke yake.” Yaani, tunawezaje kukua katika uvumilivu na saburi ikiwa hatutahitajika kungojea kile tunachokitarajia au kustahimili yale tusiyoyafurahia tukiwa katika hali ya kungojea?

Tunapojaribiwa, tunakua au angalau tunaweza kukua, iwapo tutaruhusu “saburi ifanye kazi yake kikamilifu” (Yakobo 1:4).

Uchungu, kupinga na kupakimbia mahali popote pagumu hakuleti saburi. Yakobo 1:4 (Tafsiri ya AMP) inasema tunaweza kuwa tumekomaa kikamilifu na kutokosa (au kutopungukiwa na neno kulingana na *Union*) baada ya saburi kufanya kazi yake kikamilifu. Hii ni rahisi kuelewa. Ikiwa mtu ni mvumilivu kabisa, basi anaweza kuwa na amani na furaha katika hali yoyote.

Mimi sijakamilika kamwe katika subira, lakini nimekua kiasi kikubwa. Kulikuwa na wakati ambapo nilikuwa sina saburi hata kidogo, na sikuwa ninangoja vyema. Mwishowe nilipata kuelewa kwamba Mungu hatabadilika, na hivyo basi nikaamua kubadilika na kujilainisha kulingana na njia zake. Yeye Anasema kwamba sisi hupokea kwa imani na subira, kwa hiyo nikaamua kuacha saburi ikue ndani yangu. *Nimekua katika saburi, na kwa kiasi kile kile, nimepokea amani na furaha.*

Saburi ni tunda la Roho. Saburi ndani yetu ni ushuhuda mkuu kwa wasio amini. Ni kama msuli, jinsi unavyohitajika kuutumia zaidi, ndivyo unavyozidi kupata nguvu zaidi. Jinsi ifanyikavyo kwa msuli ndivyo ifanyikavyo kwa subira – mwishowe, unakomaa kabisa na unahitajika kufanya mazoezi machache tu ili kujiweka katika hali yenye nguvu katika sehemu ya subira na uvumilivu. Huwa tunapata fursa ya kufanya hivyo kupitia mambo mbali mbali tofauti yanayofanyika kinyume na vile ulivyojipangia; kama vile watu wenye mwendo wa pole pole mbele yako, au gari lililo haribikia barabarani, kutoelewa ni kipi kinachofanyika maishani mwako au kuhitaji majibu yanayoonekana kuchukua muda kukufikia.

Mambo haya yote hutusaidia hatimaye, hata ingawa ni magumu tunapokuwa tunayapitia. Kama tunaweza kuona haya, tutasaidika kupata ufahamu mpya kuhusu saburi. Waebrania 12:1 (Tafsiri ya AMP) inatutia moyo kwa kusema, “Na tupige mbio kwa saburi na kustahimili, na kuendelea kwa nguvu ya kutokata tamaa katika njia iliyoteuliwa ya mashindano yaliyo mbele yetu.” Kila

mashindano ya mbio yana mwisho wake. Utafika mwisho wa mbio zako, lakini Waebrania inatuambia jinsi ya kupiga mbio hizo.

## **Jivumilie**

Niruhusu nikutie moyo uanze kuweka msingi wa kuishi maisha ya subira kwa kujivumilia. Unapofanya makosa, pokea rehema kutoka kwake Mungu na chuchumilia mwisho wa mbio zako. Kuwa na subira na kujivumilia unapoendelea kuushinda udhaifu wako. *Kukosa subira huzaa kusumbuka moyoni*, na masumbuko moyoni hutuelekeza kwenye hali ya hisia zisizo timamu, kisha tunaishia kufanya makosa mengine zaidi kuliko kama tungejipa subira kidogo pale mwanzoni.

Watu hupiga hatua za kwenda mbele kwa kasi mno wakiwa katika hali ya subira kuliko kama wako katika hali ya kusukumwa! Kuweni mkarimu katika kuonyesha subira. Itoe kwa ukarimu kwako mwenyewe na kwa wengine pia. Utapata faida zake ni za kufurahisha. Luka 8:15 (Tafsiri ya AMP) inasema, “endelea kuzaa matunda kwa uvumilivu.”



# 9



## NDOTO YANGU ITATIMIA LINI?

Ndoto yako iko kwenye harakati ya kutimia hata sasa hivi! Iko kwenye jiko inapikika. Umesikia usemi ule kwamba, “Nyungu uingojeayo haitokoti.” Nakutia moyo uishi kila siku kwa ukamilifu. Fanya sehemu yako lakini usijaribu kufanya sehemu ya Mungu.

Kunao wakati mkamilifu – wakati ulioteuliwa na Mungu. Ni Yeye tu ajuaye wakati huo ni upi. Mheshimu Mungu kwa kumtumainia, na ukiwa unasafiri kwenye njia ya kuelekea kutimilika kwa yale unayoyatarajia, *furahia safari yenyewe!*

Hakuna yeyote anayeweza kukueleza kwa hakika ni lini ndoto yako itatimia, lakini kuwa na uhakika kwamba itatimilika kwa wakati mwafaka.

*Amini hayo na uingie katika pumziko la Mungu!*

# JINSI YA KUPOKEA MAISHA MAPYA



Kama hujawahi kumkaribisha Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wako, nakualika kufanya hivyo sasa. Unaweza kuomba ombi hili, na ikiwa kweli utamaanisha unachofanya, utapokea maisha mapya katika Kristo.

*Baba Mungu,*

*Ninaamini Yesu Kristo ni Mwana wako, Mwokozi wa ulimwengu. Ninaamini alinifia msalabani na alizibeba dhambi zangu zote. Alienda jehanamu badala yangu na kuyashinda mauti na kaburi. Ninaamini Yesu alifufuka kutoka kwa wafu na sasa amekaa mkono wako wa kulia. Ninakuhitaji Yesu. Nisamehe dhambi zangu, niokoe, njoo uishi ndani yangu. Ninataka kuzaliwa mara ya pili.*

Sasa amini Yesu anaishi moyoni mwako. Umesamehewa na kufanywa mwenye haki, na Yesu atakaporudi, utaenda mbiguni. Pata kanisa zuri mabalo linafundisha neno la Mungu na uanze kukua katika Kristo. Hakuna lolote likalo badilika maishani mwako bila wewe kulifahamu neno la Mungu.

*Mpendwa,*

*Yohana 8:31, 32 inasema, "Ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanfunzi wangu kweli kweli; tena mtaifahamu kweli, nayo iyo kweli itawaweka huru."*

*Nakushawishi kulishikilia neno la Mungu, ulipande katika kilindi cha moyo wako, na kulingana na 2 Wakorintho 3:18, unavyoendelea kulitazama neno la Mungu, utabadilishwa na kufanyika sura Yesu Kristo. Andika barua ya kutufahamisha kwamba umempokea Yesu, na omba kitabu kitakacho kujia bure kuhusu jinsi ya kuanza maisha yako mapya katika Kristo.*

*Na Upendo,*

*Joyce*

# KUHUSU MWANDISHI



Joyce Meyer amekuwa akifundisha Neno la Mungu tangu mwaka wa 1976 na amekuwa katika huduma tangu mwaka wa 1980. Kabla ya hayo alikuwa Mchungaji msaidizi katika kanisa la Life Christian Centre huko St. Louis, Missouri, na alianzisha na kushirikisha mpango wa mkutano wa kila wiki ambao ulijulikana kama “Uzima ndani ya Neno (Life in the Word)”. Baada ya muda wa miaka mitano, Bwana alikamilisha mpango huo, na kumuongoza kuanzisha huduma yake na akaiita “ Life in The Word, Inc.”

Sasa, kipindi chake cha *Life in The Word* hupeperushwa kupitia Redio na Televisheni na husikika na kuonekana na mamilioni ya watu kote Marekani na ulimwenguni. Kanda zake husikizwa kimataifa, na husafiri sana akifundisha neno kupitia huduma ya *Life in The Word*.

Joyce na mumewe Dave, ambaye ndiye msimamizi wa shughuli za huduma ya Life In the Word, wameoana kwa muda zaidi ya miaka 34. Wanaishi St. Louis Missouri, na wana watoto wanne. Watoto wote wameoa na kuolewa na wote wanafanya huduma pamoja na Dave na Joyce.

Akiamini kwamba wito wake ni kuwastawisha waumini katika neno la Mungu, Joyce anasema “Yesu Alikufa kuwaweka huru waliosetwa, na Wakristo wengi hawana ushindi au wanashindwa katika maisha yao ya kila siku.” Alijipata katika hali hii miaka mingi iliyopita na baada ya kupata uhuru wa kuishi maisha ya ushindi kupitia Neno la Mungu, Joyce sasa hutembea hapa na

pale akiwa amejitandaa kuweka huru waliosetwa na kubadili hali ya huzuni kuwa ya furaha. Anaamini kwamba kila mtu anayeishi maisha ya ushindi apaswa kuwasaidia wengine kuishi maisha kama hayo. Maisha yake ni ya uwazi, na mafundisho yake ni rahisi na ya kueleweka yanayoweza kutumika katika maisha ya kila siku.

Joyce amefundisha kuhusu uponyaji wa hisia na mafundisho mengine yanayoandamana na hayo katika mikutano yake yote nchini Amerika, akiwasaidia maelfu. Amenakili zaidi ya kanda za redio 225 na zaidi ya kanda 70 za Video. Ameandika zaidi ya vitabu 45 kusaidia mwili wa Kristo kuhusiana na mada tofauti tofauti.

Mafunzo yake kuhusu “Uponyaji wa Hisia” yanachukua zaidi ya masaa 23. Mafundisho hayo yanajumuisha kanda kama “Ujasiri”, “Urembo badala ya Majivu”; “Kumilki hisia zako”; “Uchungu, Chuki, na Kutosamehe”; “Mzizi wa Kukataliwa”; na kanda ya dakika 90 ya vifungu vya Biblia na muziki iitwayo “ Uponyaji wa moyo uliovunjika.”